# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SITA

### Kikao cha Tatu – Tarehe 2 Februari, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilisha Mezani, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):-**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 44 la tarehe 21/10/2016
(ii) Toleo Na. 45 la tarehe 28/10/2016
(iii) Toleo Na. 46 la tarehe 04/11/2016
(iv) Toleo Na. 47 la tarehe 11/11/2016
(v) Toleo Na. 48 la tarehe 18/11/2016
(vi) Toleo Na. 49 la tarehe 25/11/2016
(vii) Toleo Na. 50 la tarehe 02/12/2016
(viii) Toleo Na. 51 la tarehe 09/12/2016

(ix) Toleo Na. 52 la tarehe 16/12/2016
(x) Toleo Na. 53 la tarehe 23/12/2016
(xi) Toleo Na. 54 la tarehe 30/12/2016
(xii) Toleo Na. 01 la tarehe 06/01/2017
(xiii) Toleo Na. 03 la tarehe 20/01/2017

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu kwenye sehemu ya kusemea kwa ajili ya maswali.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya Waheshimiwa Wabunge walioomba kuuliza maswali. Tutaanza na Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq. *(Kicheko)*

Samahani nilikuwa sijakuona, Mheshimiwa Mbowe.

Mheshimiwa Halima, uwe unatulia kidogo, tafadhali!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona lakini nilisikitika kwamba unadai hujaniona, lakini nashukuru umeniona hatimaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali la msingi la kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni siku ambayo Taifa letu linaadhimisha siku ya Haki Duniani. Tunapoadhimisha siku hii ya Haki Duniani ambayo nina hakika leo Spika wetu yupo Dar es Salaam kwa ajili ya jukumu hilo akiungana na viongozi wengine wa Kitaifa akiwemo Mheshimiwa Rais na Jaji Mkuu. Ni miezi mitatu kamili tangu Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha akamatwe nje ya geti la Bunge na kupelekwa kizuizini kushtakiwa kwa kesi inayoitwa ya uchochezi ambayo ina dhamana, lakini miezi mitatu leo hajaweza kupata dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tuna Mbunge mwingine wa Kilombero, Mheshimiwa Lijualikali ambaye anatumikia kifungo cha miezi sita

katika Gereza la Ukonga kule Dar es Salaam na kazi ngumu; wakati huo huo, tuna zaidi ya Madiwani sita wa Chama cha CHADEMA ambao wamefungwa kwa makosa yenye misingi ya kisiasa; tuna viongozi kama Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa wa Lindi aliyefungwa miezi nane kwa kufanya kazi yake ya kisiasa.  Tuna viongozi wa ngazi mbalimbali zaidi ya 215 aidha wamefungwa ama wanaendelea na mashtaka mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona namna Serikali inavyotumiwa mawakala na vibaraka wake kukigawa na kukidhoofisha Chama cha Wananchi *(CUF)* ikiwemo kumtumia Msajili wa Vyama vya Siasa kudhoofisha Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, maadam Mheshimiwa Rais alishatangaza kwamba kusudio lake ni kufuta vyama vya upinzani kabla ya mwaka 2020, haya yanayoendelea katika Awamu ya Tano ambacho ni kinyume na utamaduni na mazoea yetu kama Taifa, ni sera au utekelezaji wa sera hiyo ya kuua upinzani; na ni sera chini ya Serikali yako na Mheshimiwa Magufuli? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, katika maelezo yako marefu, yameingia huko maswali ya kisera na maswali ya kisheria. Maswali yanayohusu Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Lijualikali na Madiwani sita uliosema wamefungwa, yale ni maswali ya kisheria. *(Makofi)*

Maswali uliyouliza ya jumla kuhusu leo kuwa siku ya Haki Duniani ambayo ni Siku ya Sheria Duniani, hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kuyajibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Acha Waziri Mkuu ajibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ajili ya maswali ya kisera na siyo ya watu mahsusi aliowataja ambayo yanahusu sheria.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufafanua maswali yangu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, nimeshamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya majibu. Naomba ukae tafadhali, nimeshamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Kelele)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nikanushe kwamba Mheshimiwa Rais hajawahi kutangaza kuvifuta Vyama Vya Upinzani. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, naomba uzime *microphone* yako.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Spika umesema kwamba Watanzania wote wanajua kwamba nchi hii inaongozwa kwa sheria, kanuni na taratibu, lakini pia tunajua katika kuendesha nchi tunaendesha kwa mihimili mitatu. Iko Serikali, Mahakama na Bunge. Hakuna mhimili unaoweza kuingilia mhimili mwingine. *(Makofi)*

Tatu, Watanzania wote wanajua kwamba jambo lolote ambalo liko Mahakamani haliwezi kuzungumzwa mahali pengine popote. Kwa hiyo, siwezi kutumia nafasi hii kuzungumzia mambo yote yaliyoendelea chini ya sheria na yaliyoko Mahakamani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, swali la nyongeza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kauli kwamba Rais ameshawahi kutamka kwamba anakusudia kuhakikisha *by 2020* hakuna upinzani, ni kauli iliyotolewa na Rais. *(Makofi)*

Na kwa sababu ni kauli iliyotolewa na Rais na kwa sababu Rais huyu ambaye Mheshimiwa Waziri Mkuu umekiri katika majibu yako hapa kwamba nchi yetu inaendeshwa kwa Sheria na Katiba, ameonekana mtu wa kuvunja Katiba mara kwa mara ikiwemo kupiga marufuku mikutano vya vyama vya siasa, jambo ambalo ni haki ya vyama vya siasa ya Kikatiba.

Je, Waziri Mkuu tukileta ushahidi katika Bunge hili la Rais kutoa kauli za kukusudia kutokuwepo upinzani mwaka 2020, utakuwa tayari kuwajibika kwa kujiuzulu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, maelezo uliyoyatoa…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Naomba tusikilizane kama ambavyo mnamsikiliza Kiongozi wenu akiwa anazungumza. Naomba tusikilizane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbowe swali lako la maelezo ya kijumla yako sawa sawa. Swali lako la kumtaka Waziri Mkuu kuwajibika siyo la kisera. Kwa hiyo, uliza swali…

**MBUNGE FULANI:** Hivi haya ni maswali kwa Waziri Mkuu au ni maswali kwako?

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu umemwuliza kama Waziri Mkuu atakuwa tayari kuwajibika. Hiyo ni sera gani? Hiyo siyo sera. Uliza swali la kisera.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ya Utawala Bora. *(Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** La utawala bora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe naomba uulize swali la kisera kwenye hayo hayo maelezo uliyoyatoa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, labda nili-*address* swali hili zaidi kwa Mheshimiwa Naibu Spika.

Swali langu lilikuwa ni *follow up question* na *follow up question* yoyote inatokana na majibu ya msingi yaliyotolewa. Sasa kama kulikuwa kuna msingi wa kisera katika swali la msingi, *a follow up question* ina-*respond* kwa majibu yaliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waziri Mkuu ambaye amesema kwamba Mheshimiwa Rais hajawahi kutamka popote wala kusema popote anakusudia kuua upinzani, tumletee ushahidi ndani ya Bunge hili na kama ushahidi huo ukidhihirika kwamba ni kweli Mheshimiwa Rais ametenda na amezungumza maneno hayo, basi kwa sababu kuzungumza uongo ama kauli zisizokuwa za kweli ni katazo la kikanuni la Bunge; Waziri Mkuu achukue nafasi yake ya kuwajibika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbowe. Waheshimiwa Wabunge, lazima tufuate utaratibu tuliojiwekea wenyewe na utaraibu tuliojiwekea, suala la Waziri Mkuu kujiuzulu liko kikatiba siyo swali la sera. Kwa hiyo, tunaendelea.

Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Jibu swali hilo. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani walipiga makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, naomba uwaambie watu wako watulie. Naomba uwaambie watu wako watulie. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbowe hana watu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, kwa sababu hawa watu wako upande huu naona wanayo namna ya kutaka kusikiliza maelezo ya kwako tu na siyo mtu mwingine. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hakuna mtu wa mtu hapa!

**NAIBU SPIKA:** Naomba uwaambie watulie ili tuweze kuendelea na utaratibu uliyo mbele yetu. Nakuruhusu uongee nao.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa… *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kauli tunazozizungumza sisi na inawezekana maumivu yanayopatikana upande huu huyaelewi. Kwa hiyo, tunapoomba watawala waelewe *demise* inayopatikana upande wa *opposition* na mateso wanayopata Watanzania wenzenu, unaonekana Naibu Spika hutaki jambo hili lizungumzwe ili litafutiwe ufumbuzi. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa watu hawa ambao aidha ni wafungwa watarajiwa ama tayari ni wafungwa wazoefu na wengine walioko nje ambao wanateswa kutokana na utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano kutaka kuua demokrasia katika Taifa hili, ninyi kama Bunge upande wa wenzetu wa pili katika Bunge hamlioni hili kama tatizo; na tunapotoa kauli za kuomba *remedy* hamzioni; ni kwamba ninyi mnabariki jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye namheshimu sana, atoe Kauli ya Serikali. Kama siyo sera, basi atusaidie kwamba tunatokaje hapa ili turejeshe nchi hii katika misingi ya demokrasia ambayo imeheshimiwa kwa miaka mingi kulijenga Taifa hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naona umesaidia kwa sababu walitulia kukusikiliza. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Saddiq.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina swali moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa waziri Mkuu, kwa kuwa mwaka 2016 miezi kama hii kulitokea upungufu mkubwa wa sukari nchini …

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Haya mambo haya!

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** … na Serikali ya Awamu ya Tano ilifanya jitihada kubwa sana kukabiliana na hali ile na hatimaye nchi yetu ikapata utulivu mkubwa katika suala zima la sukari.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikupongeze wewe na Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa mliyofanya mwaka 2016 katika suala zima la upungufu wa sukari nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kipindi hiki, viwanda vyetu vya ndani vinakamilisha msimu, vingine vinamaliza mwezi wa Tatu, vingine vinamaliza mwezi wa pili; na kwa kuwa vikikamilisha msimu, uzalishaji unaanza tena mwezi wa sita na kuendelea. Je, hali ilivyo sasa ya sukari nchini ikoje? Serikali imechukua juhudi gani kuhakikisha kwamba yale yaliyotokea mwaka 2016 hayatatokea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saddiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niwahakikishie Watanzania kwamba hakutakuja kutokea upungufu wa sukari, kwa sababu viwanda vyetu vya ndani vilishaanza uzalishaji na sasa vinaendelea na uzalishaji. Tunavyo

viwanda vitano ambavyo tumevitembelea, tumehakiki utendaji kazi wake na uzalishaji upo na sukari ambayo inatumika nchini inatokana na uzalishaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaaamini kufikia mwishoni mwa msimu ambapo ni mwezi wa tatu mwaka huu wa 2017 tunaweza kuwa tumezalisha na kufikia malengo. Kwa sababu kwa taarifa za mwisho, mpaka mwishoni mwa Januari, uzalishaji kwa malengo waliokuwa wamejiwekea wamefikia asilimia 86. Asilimia iliyobaki inaweza kuzalishwa kwa kipindi kifupi kilichobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama itajitokeza upungufu kwa sababu ya mahitaji ya sukari, pia kutozuia upandaji wa bei, Serikali itakuwa iko tayari kutafuta namna nzuri ya kupata sukari tukishirikiana na viwanda vyenyewe ikiwa ni mkakati wa kuvilinda viwanda vya ndani vinavyozalisha sukari ili viweze kuongeza uwezo wa uzalishaji wa sukari nchini. Huo ndiyo mpango wa Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saddiq, swali la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa majibu hayo. Kwa kuwa viwanda vya ndani vimejipanga, na kiwanda cha sukari Mtibwa ambacho kiko katika Jimbo la Mvomero na Wilaya ya Mvomero kimejipanga vizuri sana. Je, Serikali iko tayari kuvisaidia sasa viwanda hivi vya ndani ili viweze kukamilisha lengo la Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saddiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, wakati wote tumekuwa tukiendesha mazungumzo kati ya viwanda vyote vya ndani ikiwemo vya sukari, namna bora ya kuongeza uzalishaji wa bidhaa zao na bidhaa zenye ubora kwa namna ambayo Serikali inaweza na utayari wake iliyonao, kuvisaidia viwanda hivi kuweza kuzalisha zaidi. Kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi, Serikali imekaa mara nyingi na wazalishaji wa sukari, kuona mwenendo wa uendeshaji wa viwanda vyao na uzalishaji wake, kupata changamoto zinazowakabili kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imedhamiria kulinda viwanda vya ndani na kusaidia uzalishaji mpana, tunao mpango na tumeandaa pia njia nzuri ya viwanda hivi kupata msaada wa kuendelea kuzalisha ikiwemo kupata

mitaji, kupitia mabenki tuliyonayo na pia kuhamasisha wakulima wanaolima jirani ili waweze kuzalisha mazao yanayofanana na yale ili kuongeza uzalishaji. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuwa pamoja na wazalishaji ili kuweza kuzalisha zaidi zao la sukari.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mujibu wa taratibu za kisera tulizonazo, Serikali ina wajibu wa kuangalia hali ya chakula nchini. Kwa taarifa ya Serikali, Halmashauri 55 zina upungufu wa chakula. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuleta chakula ili kupunguza mfumuko wa bei ulioko sokoni sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la chakula limeelezwa vizuri sana na Waziri wa Kilimo kupitia taarifa Bungeni juzi na taarifa yake imefafanua vizuri na hatua ambazo Serikali inazichukua za kuhakikisha kwamba Watanzania wanaendelea kuwa na akiba ya kutosha kwenye maeneo yao ili Watanzania waweze kuwa na uwezo wa kuendelea na uzalishaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikusudii kurudia maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini Serikali inaendelea kuwahamasisha wafanyabiashara wa ndani pia kutumia nafasi hii kufanya biashara kutoka Wilaya moja ambayo ni kwenye mazao mengi kwenda maeneo mengine ili kuweza kuongeza idadi ya chakula na kupunguza bei kwenye masoko na tunao ushahidi wa kutosha kwamba Mikoa ya Rukwa, Mbeya Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma bado ina chakula cha ziada, lakini pia hata kwenye soko letu la Kimataifa - Kibaigwa kuna mahindi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wafanyabiashara wa ndani watumie nafasi hiyo kuweza kuchukua chakula na kupeleka kwenye maeneo ambayo yana upungufu. Hata jana tulikuwa tunazungumza pia na Mheshimiwa Mathayo, Mbunge wa Same Mashariki namna ambavyo Same imekuwa kame wakati wote, hata msimu ambao tunakuwa na mvua nyingi, kuona namna nzuri ambayo tunaweza kuwasaidia kupata chakula kwa kutumia pia hata wafanyabiashara wa ndani zaidi ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeanza kushuhudia kuona mvua zikinyesha ingawa siyo nyingi za kutosha, lakini basi pale ambako tunapata mvua angalau mara moja, mara mbili, tunawahamasisha wakulima kulima mazao ya muda mfupi ili yaweze kuiva kwa kipindi kifupi pia tuweze kujipatia chakula kwa msimu ujao wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kutakuwa na tatizo lolote lile, Serikali hii iko bado inajua na inafuatilia mwenendo wa hali ya chakula na ufumbuzi tutaupata kupitia Serikali yenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Destery, swali la nyongeza.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Waziri Mkuu kwa ufafanuzi mzuri na ambao kweli ulitolewa na Waziri wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunayo makundi mawili, kundi ambalo lina uwezo wa kifedha lakini bei iko juu na utaratibu wa Serikali ni kuwapelekea ili kwenda kupunguza mfumuko wa bei, lakini tunalo kundi pia ambalo lilitajwa na Waziri wa Kilimo, kaya kama 3,000 hivi ambazo zina hali mbaya na hazina uwezo hata wa kununua chakula. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba jambo hili linaenda kuwasidia wananchi wake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwezo mkubwa, mdogo au wa kati wa kifedha ni jambo pana ambalo kila mmoja na katika kila familia inayo utaratibu wa kujiongezea uchumi kwenye maeneo yao badala ya Serikali kuwaahidi kwamba tutawapelekea fedha ili kuwaongezea fedha; na kwa kuwa tumesema chakula sasa kinapanda kwenye masoko, ni kweli, lakini ni kwa sababu ya hofu ya hali ya hewa ambayo tunayo ya msimu huu wa kilimo, watu wengi wameweka chakula ndani wakidhani, kutumia nafasi hiyo wanaweza kujipatia fedha nyingi. Jambo hili halikubaliki kimsingi kwa sababu tunawaumiza wale ambao wana kipato cha chini kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama hali ya chakula inakuwa nzuri, bado tuna kundi la watu ambao hawana uwezo wa kifedha. Muhimu zaidi watanzania wote tutambue umuhimu wa kila mmoja kuwa lazima apate chakula, aweze kupata mavazi, aweze kupata malazi kwa kile kidogo alichonacho.

Kwa hiyo, wafanyabiashara wetu nawasihi sana, tusijenge tabia ya kupandisha bei vyakula au bidhaa zetu bila sababu yoyote ile ili iweze kuwawezesha wale wote ambao wamezoea kuishi katika maisha ya kawaida, maisha ya kati na wale wapate chakula, waweze kupata huduma nyingine ili pia waweze kuendesha maisha yao. Huo ndiyo msingi imara wa jambo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, ni vizuri ukiweza kutulia kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuangalia muda wetu pale, hatutaweza kuendelea na maswali kwa sababu tuna dakika mbili na hazitaweza kutupa swali na kupata majibu mazuri kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Katibu. *(Makofi)*

**NDG. ZAINABU ISSA - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 31

### Uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 Sehemu ya Tatu, kifungu cha 8 kinaelezea uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na kifungu cha 13 kinazungumzia vyanzo vya fedha.

(a) Je, ni kwa nini baraza hilo halifanyi kazi kama sheria inavyoelekeza?

(b) Sehemu ya Tatu ya kifungu cha 14 cha sheria hiyo kinaeleza juu ya Kamati za Watu Wenye Ulemavu kuanzia ngazi ya kijiji; je, ni kwa nini Kamati hizo mpaka sasa hazijaundwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex , Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Ushauri la Utaifa la Watu wenye Ulemavu limeanzishwa chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010. Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu lilizinduliwa rasmi tarehe 1 Novemba, 2014. Baraza hili limekuwa likifanya kazi ipasavyo kwa kujadili masuala ya watu wenye ulemavu kupitia vikao vyake ambapo kwa mara ya mwisho Baraza lilikutana tarehe 14 Januari, 2017.

Aidha, Baraza limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa kuishauri Serikali kuhusu uboreshaji wa huduma za watu wenye ulemavu nchini.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Watu wenye Ulemavu, kifungu cha 14(2) inaelekeza kuundwa kwa Kamati za Watu wenye Ulemavu katika ngazi ya Kijiji/Mtaa, Kata, Halmashauri hadi Mkoa.

Kutokana na kifungu hiki cha sheria, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imekwishatoa agizo kwa Mikoa na Halmashauri zote chini kuunda Kamati za Watu Wenye Ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuikumbusha Mikoa na Halmashauri ambazo hazijaunda Kamati za Watu Wenye Ulemavu kutekeleza agizo hilo kwani ifahamike kwamba kutokuunda kamati hizo ni ukiukwaji wa matakwa ya kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Baraza hili limekuwa likifanya kazi kwa kusuasua sana. Kisheria linatakiwa lifanye kazi, ama likutane, ama lifanye vikao vyako japo mara nne kwa mwaka, jambo ambalo halijawahi kutokea.

Je, ni nini *commitment* ya Serikali kuhakikisha kwamba Baraza hili linakutana, ama linafanya vikao vyake kama sheria inavyolitaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, agizo la kuundwa kwa hizi Kamati kuanzia ngazi ya Vijiji mpaka Mkoa, ni agizo ambalo limetolewa mara kadhaa lakini kamatii hizi haziundwi. Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muda muafaka wa kutoa *deadline* ya uundwaji wa Kamati hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010, Mabaraza haya yanatakiwa kukaa mara nne kwa mwaka. Sheria Na. 9 ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010 imeanza kutekelezwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya sheria hii, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 1982 ilizungumza pia kuhusu Mabaraza haya. Wakati wa Tume ya Marekebisho ya Sheria walipokuwa wakiangalia Sheria za Watu wenye Ulemavu waligundua kwamba mabaraza haya hayakukaa kwa muda mrefu sana, takribani miaka kumi na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia, katika utekelezaji wa sheria hii, ndani ya mwaka mmoja, tayari Mabaraza haya yameshakaa na yameanza kutoa ushauri kwa Serikali. Baraza la kwanza lilikaa mwaka 2016 mwezi wa nne ambalo alifungua Mheshimiwa Dkt. Possi na Baraza la pili tayari limekaa tarehe 14 Januari, 2017. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha mabaraza haya yanakaa kwa mujibu wa taratibu kama ilivyoelezwa kwenye sheria na tutaendelea kuitengea fedha ili watu wenye ulemavu wapate fursa ya kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mabaraza haya, Serikali imekuwa ikipata ushauri mbalimbali na sisi tumekuwa tukiyafanyia utekelezaji hasa kupata ushauri kutoka kwenye haya mabaraza.

Mheshimiwa Ikupa, jambo moja tu la ziada, ukisoma kwenye sheria yetu kifungu namba 46(1)(b) kimetoa mazingira ya kusaidia mafunzo ya ufundi stadi kwa watu wenye ulemavu ambayo imekuwa ni mapendekezo ya baraza hili. Na sisi katika utaratibu wetu, tumeshazungumza na watu wa *VETA* na wamesha-

*mainstream* mfumo wa utoaji wa mafunzo kwa walimu wao ambapo kwa sasa hivi wanafundishwa elimu ya msingi kabisa ya kuwafundisha watu wenye ulemavu. Lengo letu ni kuweza kuwafikia wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili tunao ushahidi wa mtu mwenye ulemavu, ndugu yetu mmoja anaitwa Boniface Kayenzi, ana umri wa miaka 63, amefundishwa *VETA*, sasa hivi anatengeneza na kuranda mbao na amekuwa akitumiwa katika sehemu mbalimbali za Maonesho ya Kimataifa na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, amezungumzia kuhusu uundwaji wa Kamati hizi za watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya Kata mpaka huku juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mujibu wa sheria yetu, kuna kitu kinaitwa *sectorial plan* ambapo inafanya kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara nyingine. Mheshimiwa Waziri wa Nchi alikwishaandika barua Ofisi ya Rais - TAMISEMI), ambapo kule chini ndiko wanakosimamia hizi Kamati, kwa maana ya Halmashauri na Mikoa ili sasa agizo hilo lishuke chini. Mheshimiwa Simbachawene alikwisha kuiandika barua hiyo kufika chini ili Kamati hizi ziundwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge, niwaombe tu na Wabunge wote mlioko hapa, sisi Wabunge tunapata fursa kuingia kwenye vikao vya Halmashauri, mtusaidie na ninyi katika vikao vyetu kuendelea kutoa msisitizo ili Kamati hizi ziweze kuundwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona, na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu *(UNCRPD),* na mkataba ule unazitaka nchi zilizoridhia mkataba huo kutekeleza, kutatua na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wenye ulemavu. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Mfuko wa Watu wenye Ulemavu haukutengewa kabisa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anatueleza nini kuhusiana na mfuko huu ambao haukutengewa fedha zozote na kwa sababu hakuna fedha, inazokwamisha pia hili Baraza la Watu wenye Ulemavu kushindwa kutimiza wajibu wake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Sera ya Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004, vilevile na *United*

*Nations Conventions of Rights of People with Disabilities* na yenyewe imesema namna ya kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum hasa katika kundi hili la walemavu katika kuwasaidia kuboresha maisha yao na shughuli zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hapo katikati hakukuwepo na fedha za kutosha katika mfuko huu kuwezesha kufanya shughuli zake. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge, ya kwamba kwa sasa katika bajeti inayokuja ya mwaka 2017/2018, tumeona umuhimu huo na tumeshaanza kuandaa mapendekezo ya kupeleka katika bajeti yetu hiyo ili sasa mfuko huu uwezeshwe na uweze kukidhi mahitaji na utekelezaji wa mfuko huu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuondoe tu hofu ya kwamba tunafahamu changamoto hiyo ya fedha lakini tumejiandaa *this time* tuitengee fedha ili iweze kufanya kazi yake kikamilifu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Mpango wa Kuzuia Athari Zinazosababishwa na Tetemeko la Ardhi**

**MHE. MBAROUK SALIM ALI** aliuliza:-

Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizomo katika Bonde la Ufa pamoja na milima mikubwa; kutokana na hali hiyo, upo uwezekano mkubwa wa kutokea kwa matukio kama tetemeko la ardhi mara kwa mara kama ambavyo imeshaanza kutokea na kuleta athari kubwa kwa Taifa.

Je, Serikali ina mkakati gani iliyojiwekea wa kuzuia au kupunguza athari pale inapotokea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa nchi yetu kama zilivyo nchi nyingine imekuwa ikikumbwa na majanga mbalimbali ya asili na yale yanayosababishwa na shughuli za binadamu na kusababisha athari kubwa kwa Taifa letu. Miongoni mwa majanga hayo ni tetemeko la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua uwezekano wa kutokea kwa majanga haya, imejiwekea mikakati mbalimbali ya kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea. Aidha, kwa vile maafa ya asili kama vile tetemeko la ardhi ni vigumu kuyatabiri, Serikali kupitia Wakala wa Jiolojia imekuwa ikitoa elimu kwa umma juu ya kukabiliana nayo kwa lengo la kupunguza athari pindi yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeandaa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ambayo imeainisha aina mbalimbali za maafa ikiwemo tetemeko la ardhi pamoja na jukumu la kila mdau katika kushughulikia masuala ya maafa. Vilevile Serikali imeandaa Mwongozo wa Taifa wa kukabiliana na maafa ambao unaelekeza taasisi ongozi wajibu wao katika kukabili maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mkakati kiongozi wa kudumu katika kuhakikisha kwamba suala la Menejimenti ya Maafa inatekelezwa, Serikali imetunga Sheria mpya ya Menejimenti ya Maafa Na. 7 ya mwaka 2015 ambayo pamoja na kusimamia mikakati ya kudumu ya kukabiliana na maafa, imeelekeza kuundwa kwa Kamati za Maafa katika ngazi mbalimbali. Moja kati ya wajibu wa Kamati hizi ni kuhakikisha zinafanya tathmini za kubaini maeneo ambayo yako katika hatari ya kukumbwa na maafa na zinaweka na kupendekeza mikakati ya kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile suala la maafa ni mtambuka, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo *(development partners)*, pamoja na Chuo Kikuu cha Ardhi, ilifanya tathmini ya kuainisha maeneo yenye viashiria vya uwezekano wa kukabiliwa na majanga mbalimbali *(vulnerability assessment)* ambayo ilifanyika nchi nzima. Baada ya kuona ukubwa wa tatizo

hili, Serikali iliandaa Mpango wa Taifa wa kujiandaa na kukabiliana na maafa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kusisitiza kuwa kila mmoja wetu achukue tahadhari kwa kusikiliza ushauri unaotolewa na watalaam wetu katika kukabiliana na maafa. Hii ni pamoja na kujenga nyumba katika maeneo yaliyopimwa na salama kwa kuishi, lakini vilevile kwa kuzingatia viwango sahihi vya ujenzi *(building codes)* kulingana na maeneo tunayojenga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, swali la nyongeza.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri na mtiririko mkubwa wa mikakati na Kamati ambazo zimeundwa, lakini pia nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, pamoja na mikakati na kamati nyingi ambazo zimeundwa, lakini uzoefu wa tetemeko la ardhi la Kagera na hili balaa la njaa linaloendelea sasa hivi nchini kote, inaonekana kwamba Serikali inapiga tikitaka jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua, kwa sababu mikakati ni jambo moja, lakini pia na utayari. Sasa nataka kujua utayari wa Serikali juu ya kukabiliana na majanga kama hayo yanapotekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna tetesi kwamba kwenye miaka ya 1980 kuliwekwa vifaa katika baadhi ya maeneo ya hapa nchini ikiwemo Mbeya, nafikiri na Dodoma na Arusha. Nilitaka kujua uwepo wa vifaa hivyo, lakini pia na shughuli ambazo vinafanya kwa sasa? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, swali lake la kwanza ameuliza utayari wa Serikali kukabiliana na majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi nimesema, imeundwa sheria makusudi kabisa kwa ajili ya kukabiliana na jambo hili, lakini ndani ya sheria imetengenezwa miongozo zaidi ya minne ambayo imetawanywa nchi nzima katika maeneo tofauti tofauti.

Lengo la hizi Kamati ni kwamba kupitia miongozo ile, kila maeneo na baada ya kuwa ilishafanyika *assessment* yako baadhi ya maeneo ambayo ni *vulnerable,* ambayo yako *prone* kwenye majanga, hasa hilo tetemeko la ardhi; na Mheshimiwa Mbunge kwa mujibu wa tafiti za kijiolojia zinasema, kwa mwaka mmoja duniani kote yanatokea matetemeko ya ardhi kuanzia 150 mpaka 1,500 ambayo yana nguvu za mtetemo kwa kipimo cha *richter* 4.5 mpaka 5.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mazingira yetu haya na sisi tumeandaa utaratibu huo kupitia miongozo yetu ili kuwafanya watu wetu wawe tayari muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba kupitia Kitengo cha Maafa, utaratibu huu umewekwa na kutokana na *experience* mbalimbali sasa tunajiandaa kukiboresha kitengo hiki ili kiendane na hali ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili limeuliza kuhusu vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya matetemeko ya ardhi yanasimamiwa chini ya Wakala wa Jiolojia Tanzania, ambayo ni *GST*. Ninavyozungumza hivi sasa, katika maeneo yale yote ambayo yako *prone* na suala hili la matetemeko, tayari tuna vituo tisa hivi sasa tunavyozungumza; katika Mkoa wa Dodoma, Geita, Singida, Kibaya, Kondoa, Mbeya na Mtwara na vituo hivi vinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba vituo hivi vipo na vinafanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lwakatare, swali la nyongeza.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Swali langu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza hivi sasa wananchi wa *Bukoba Town* ambao walipata matatizo ya tetemeko, wako katika shida. Mbaya zaidi ni kwamba pamoja na miongozo, kamati hizo, mikakati tunayoizungumza, imepelekea kuona hiyo miongozo haiwasaidii, kwa sababu, hadi hivi sasa pamoja na miongozo na Kamati zenu ni kwamba hata misaada ambayo wamepewa au kuelekezewa na mashirika na taasisi mbalimbali ikiwemo Bunge hili, bado hawajapata misaada hiyo. Hebu uhakikishe hiyo miongozo inawaondolea uhalali wa kupata michango inayochangwa na taasisi

mbalimbali, likiwemo hata Bunge hili lililowachangia, lakini misaada hawakuipata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo tuliyoitoa ilikuwa ni miongozo ambayo inasaidia katika masuala yote ya maafa na zile Kamati zipo kwa ajili ya jambo hilo. Sasa kwa kesi ya Bukoba, michango iliyotolewa na taasisi mbalimbali likiwemo Bunge hili; na ukisoma hata katika *Hansard* ya tarehe 13 Septemba, 2016 wakati hoja ya Mheshimiwa Shangazi imesemwa hapa ya kuchangia, maelezo ya mwisho hayakusema michango ile inakwenda kufanya shughuli gani, lakini ilisema michango ile…

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa!

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipaza sauti)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** ...ilisema michango ile ni kwa ajili ya waathirika, kwa maana ya wahanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa twendeni pole pole. Mwisho wa siku…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri ya kujibu. Tuache kumuongelesha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku, maelekezo yalikuwa ni fedha hizi ziende zikawaguse wale ambao wameathirika (wahanga). Wakati huo huo, katika Kiti cha Waziri Mkuu hapa, alikuwepo Mheshimiwa Lukuvi kama Kaimu na alitoa tamko la Serikali kwamba fedha hizi zitawafikia wahanga, kwa maana ya wale ambao wameathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa turudi katika hoja ya msingi. Serikali ikijenga hospitali, Serikali ikiboresha shule ambazo zimebomoka, mwisho wa siku anayekwenda kuhudumiwa ni yule muhanga ambaye ni mwathirika. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba fedha hizi hazijawafikia walengwa. Zimewafikia walengwa kupitia katika huduma za hospitali na katika mashule.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, sasa aulize swali lake.

Na. 33

**Kuongeza Maeneo ya Vijiji Vilivyotangazwa Mwaka 1974**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Halmashauri ya Nsimbo imekuwa ikipokea wahamiaji toka mikoa mbalimbali ambao ni wakulima na wafugaji na kusababisha kukosa maeneo yenye rutuba.

Je, ni lini Serikali itaongeza maeneo ya vijiji vilivyotangazwa mwaka 1974?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote vilivyoanzishwa mwaka 1974 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Katavi na Msitu wa Hifadhi wa Msaginya, *Mulele Hills* na *Mpanda North East.* Misitu hii pamoja na Mbuga ya Katavi iko chini ya usimamizi wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi za Taifa zipo kwa mujibu wa Sheria kwa maslahi mapana ya Taifa zima na hairuhusiwi kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo hayo yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, endapo kuna hoja ya kuongeza eneo la kijiji kwa kumega eneo la hifadhi, kijiji kinatakiwa kwanza kuanza mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuainisha takwimu za msingi za idadi ya watu, idadi ya kaya, ukubwa wa eneo lililopo na mahitaji ya ardhi ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyenye mahitaji ya ardhi kutoka kwenye hifadhi vinatakiwa kujadili suala hili katika Mikutano Mikuu ya Vijiji, Kamati ya

Maendeleo ya Kata, Kamati ya Ushauri ya Mkoa na hatimaye maombi hayo kuwasilishwa Wizara yenye dhamana na kuwasilishwa kwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa viongozi wa Vijiji, Wilaya na Mkoa, kuweka utaratibu wa kudhibiti wahamiaji haramu katika maeneo ya mipakani wakiwemo wafugaji wanaoingiza mifugo katika Hifadhi za Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kwanza naomba niseme, mimi nikiwa ni Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, nina masikitiko makubwa sana kuhusiana na uongozi wa Wilaya na Mkoa kwamba katika kutekeleza majukumu yao, hawaangalii haki za msingi. Tarehe 24 wamefanya *operation* ya kuondoa watu kwenye Hifadhi ya Kijiji ambao walipewa na uongozi wa Kijiji kwa kuwachomea nyumba, mvua zinanyesha, wanakosa pa kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imekuwa ni tofauti na kauli ya Mheshimiwa Makamu wa Rais aliyotoa mwaka 2016 kwamba endapo watu wako katika maeneo ya hifadhi, wanatakiwa watafutiwe maeneo mengine na ndiyo wapelekwe. Kutokana na hilo, naomba kuuliza, je, Wizara husika iko tayari kuwafuta machozi wananchi wa Kitongoji cha Kamini, Kaumba katika Kijiji cha Katambike, Kata ya Ugala?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ilitolewa taarifa hapa kwamba imeundwa tume ambayo inashirikisha Wizara karibu tatu kushughulikia kero za migogoro ya ardhi. Sasa tunaomba majibu ya hiyo tume, yamefikia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa ilifanya uchomaji wa nyumba kwa sababu hii taarifa kwetu sisi ni mpya, ni ngeni, naomba tulichukue hili kwanza kwa ujumla wake kwa sababu jambo hili maana yake ni haki za binadamu ambao saa nyingine wameathirika. Kwa hiyo, kama Ofisi ya TAMISEMI tunasema kwamba habari hii kwanza tumeipata, tutaifanyia kazi kwanza, lakini suala zima la ulipaji wa fidia kwa wale walioathirika kwa Wizara yenye dhamana kwa sababu jambo hili, sijajua, ni

jambo mtambuka. Je, iliyohusika ni Wizara ya Maliasili na Utalii au Ofisi ya Rais - TAMISEMI?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema jambo hili kwanza lazima lifanyiwe tafiti ya kina kujua nini kilichojiri kule katika eneo hilo. Pia kuna suala zima la kikosi kazi kilichoundwa na Wizara takriban nne, je, kimefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kazi ile inaendelea hivi sasa, tukijua kwamba tuna changamoto kubwa sana nchini mwetu. Leo hii mikoa mbalimbali, ukiangalia Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Pwani na karibu katika maeneo yote kuna tatizo hilo kubwa sana. Ninaamini kabisa kikosi hicho kinaendelea na kazi hiyo na pindi taarifa hiyo itakapokuwa imekamilika ambapo aliyehitaji jambo hilo lifanyike ni Waziri Mkuu mwenyewe, basi tutapata taarifa rasmi ya Kiserikali kuhusiana na jambo hili linavyoshughulikiwa katika maeneo mbalimbali, lakini kujua ukubwa wake maana yake tunataka kuokoa Taifa hili kwa sababu sasa hivi janga la mauaji limekuwa kubwa sana, na huu ndiyo suluhu ya jambo hili kwa sababu kila eneo sasa hivi lina shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Richard Mbogo naomba tuvute subira tu, taarifa hii ikikamilika itatolewa rasmi hapa katika Bunge letu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa majibu yake mazuri, lakini nilipenda tu kuongeza jibu kwa hoja ya msingi aliyokuwa ameuliza kwenye swali la nyongeza kwamba ile Kamati iliyoundwa mpaka sasa hivi imefanya kazi wapi na wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ile Kamati mpaka sasa imeshakwenda mikoa minne; imekwenda Geita, Kagera, Morogoro na Tabora. Wakimaliza hapo, wanaelekea Kaskazini. Kwa hiyo, ile Kamati tayari imeshaanza kazi yake, lakini pia sisi ndani ya Wizara tumeshaanza kazi hiyo katika kufuatilia. Ni juzi tu nilikuwa Kusini na Waziri wangu alikuwa Kaskazini. Kwa hiyo, tunaendelea na kazi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna Kamati Maalum iliyoundwa kwa ajili ya kushughulikia matatizo hayo na wakati huo huo Kamati

inavyoendelea na kazi yake, Serikali imeendelea kuwaondoa wafugaji na kutaifisha mifugo yao, je, haioni ni wakati muafaka wa kusubiri Kamati hiyo imalize kazi yake ili waje na suluhu ya kudumu juu ya jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema, Kamati iko *site,* lakini sijajua kwa sababu wakati mwingine kuna *case by case.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine haya mambo yanatofautiana mazingira kwa mazingira; na kwa sababu katika maeneo mbalimbali tuna Wakuu wetu wa Mikoa ambao wapo; na ni viongozi Wakuu wa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mikoa hiyo, hali kadhalika na Wakuu wa Wilaya, mambo haya wakati Kamati inafanya kazi wao watapima uzito wa maeneo haya na kuona jinsi gani ya kufanya ili utaratibu uende vizuri. Lengo kubwa ni kumsaidia Mtanzania katika mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kwa sababu tuna Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya na Kamati inaendelea kufanya kazi, nawaomba Wakuu wa Wilaya kuratibu mambo haya katika maeneo yetu na mikoa yetu. Jambo kubwa ni kuwalinda wananchi wetu waweze kuishi kwa usalama ili kujenga uchumi wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Kuanza Uchimbaji - Migodi ya Liganga na Mchuchuma**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Kumekuwa kukitokea taarifa juu ya kuanza kazi ya uchimbaji katika Migodi ya Liganga na Mchuchuma.

(a) Je, ni lini kazi hiyo itaanza?

(b) Je, nini mazao ya migodi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi unganishi ya Mchuchuma na Liganga inatekelezwa na kampuni ya ubia kati ya *NDC* na *Sichuan Hongda Group Limited* ya China inayojulikana kwa jina *Tanzania China International Mineral Resources Limited.* Kampuni hii imekamilisha uchorongaji na upembuzi yakinifu wa miradi hiyo. Uchorongaji umeonesha kuwepo kwa tani milioni 428 za makaa ya mawe eneo la Mchuchuma na tani milioni 126 za chuma eneo la Liganga. Upembuzi yakinifu umeonesha Mgodi wa Chuma Liganga una uwezo wa kuzalisha tani milioni 2.9 kwa mwaka na Mgodi wa Makaa ya Mawe ulioko Mchuchuma una uwezo wa kuzalisha tani milioni tatu kwa mwaka; lakini pia uwezo wa kufua umeme wa megawati 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, gharama za uwekezaji katika miradi hii ni dola za Marekani bilioni tatu ambapo dola bilioni 600 ni mtaji wa mwekezaji na mkopo utakuwa dola bilioni 2.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni imekwishapata leseni maalum za uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe kutoka Wizara ya Nishati na Madini pamoja na vibali vya mazingira mbalimbali. Pia imepata maeneo katika eneo la Katewaka pamoja na Mchuchuma na Lupali. Kazi ya uthamini na makazi na mali ya wananchi walio ndani ya maeneo ya miradi wanaotakiwa kupisha shughuli za mradi, zimekamilika na hivi sasa tathmini ya fidia iko kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo na mwekezaji. Mradi huu utaanza mara baada ya kukamilisha fidia na wananchi waliopisha mradi pia na *Government Notice* kwa ajili ya *incentive* za mradi itakapotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo unganishi itawawezesha kuchimba makaa ya mawe kiasi cha milioni tatu na chuma ghafi tani milioni 2.9 kwa mwaka. Aidha, sehemu ya makaa ya mawe itatumika kuzalisha umeme na nyingine kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Vilevile sehemu ya chuma itatumika kwenye Sekta ya Ujenzi, Viwanda, Kilimo, na kadhalika, lakini madini ya *vanadium* yatatumika kwa ajili ya matumizi kwenye viwanda vya kemikali

pamoja na magari, lakini kadhalika madini ya *titanium* kwa ajili ya matumizi kwenye viwanda, ndege, meli, pamoja na magari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeshajionesha kwamba katika machimbo mbalimbali ya madini, wananchi wanaozunguka maeneo hayo huwa wanaathirika sana na pia wanakuwa hawana shughuli ya kufanya katika ile migodi. Sasa kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Njombe ni wananchi wanaojituma sana kwenye kilimo, je, Serikali iko tayari sasa kuanza mchakato maalum wa kusaidia wananchi wanaozunguka maeneo yale hasa Jimbo la Ludewa na Njombe Mjini, waweze kuwa tayari kuzalisha bidhaa za chakula kitaalam, pindi migodi hii itakapoanza waweze kunufaika na soko litakalokuwepo pale migodini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Mwalongo kwa jinsi anavyofuatilia kwa ukaribu suala hili kwa manufaa ya wananchi wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Serikali zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika hasa katika masuala ya *local content* kwa maana ya ushirikishwaji, Serikali imechukua hatua kadhaa; mojawapo ni pamoja na kuitaka kampuni itakayowekeza kutoa elimu pamoja na mikopo ili kuwawezesha wananchi hao kunufaika na rasilimali hiyo. Katika kazi hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nimshukuru sana, vijiji vya Itoni pamoja na Nanundu ambayo ipo katika maeneo yale, vimeshapewa elimu kwa ajili ya ulimaji wa mboga mboga, lakini pia katika shughuli za kufuga kuku pamoja na kufuga nguruwe. Kwa hiyo, wananchi wataweza kufanya kazi kwa ajili ya kujiwekeza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongeze tu kwamba Serikali kwa kushirikiana na kampuni, kampuni itaanza kutoa mikopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wanaozunguka mgodi ule kufanya shughuli ndogo ndogo za kiuwekezaji ili pia sasa waanze kushiriki mara baada ya mradi kuanza kwenye shughuli za kibiashara na za kiuchumi katika maeneo yale. Inatoa elimu, lakini

inatoa mikopo ya masharti nafuu ili wananchi waanze kufanya hivyo. Utaratibu huu ulianza tangu Oktoba, 2012 na unaendelea hadi sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda tu kuzungumza hapo kwamba tarehe 19 mwezi wa nne liliulizwa swali kwenye Bunge lako Tukufu kuwa Mradi wa Chuma, Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma, utaanza lini? Majibu ya Serikali yalikuwa kwamba kwanza fidia italipwa mwezi Juni, 2016 ambayo fidia hiyo haijalipwa mpaka leo na pili miradi hii kwamba itaanza mwezi Machi, 2017.

Je, mkanganyiko huo unatokana na nini na majibu hayo yote ambayo sasa hivi inaonekana hayajitoshelezi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa anavyosema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi. Kwenye Bunge la mwezi Aprili tulisema kwamba mradi huu utaanza mapema ifikapo mwezi Machi. Hivi sasa bado tupo Januari, hivyo Mheshimiwa Mbunge nadhani avute subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kuhusu suala la fidia; fidia inayotarajiwa kufidiwa wananchi wale inafikia takribani shilingi bilioni 13.34, ni kiasi kikubwa. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa ni kupitia tathmini halisi ya fidia hiyo, halafu baada ya zoezi hilo kukamilika, basi wananchi watalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba yapo masuala ya kimkataba ambayo Serikali pamoja na mwekezaji inayapitia, likiwemo suala la *incentives* kwa maana ya vivutio, mara baada ya kukamilika, basi mradi huu utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yetu zoezi hili likikamilika kabla ya mwezi Machi, basi kweli mradi huu utaanza mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Matumizi Sahihi ya Lugha ya Kiswahili Kwenye Vyombo vya Habari**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari hayatoi fursa ya kukua kwa lugha yetu na badala yake yanachangia kurithisha lugha yetu kwa watoto kwa namna iliyo mbovu; mathalani, Mtangazaji wa runiga au redio anasema "hichi" badala ya "hiki" au nyimbo hii badala ya "wimbo huu" na kadhalika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kimkakati wa kuvifanya vyombo vya habari kuwa mawakala wa kulinda usahihi wa lugha ya Kiswahili badala ya kuwa miongoni mwa wabomoaji wa lugha yetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu matumizi ya Kiswahili fasaha kwa vyombo vya habari. Hivi sasa inaandaliwa Sera ya Lugha ambayo itabainisha majukumu ya vyombo vya habari katika matumizi na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha, kwa sasa hatua mbalimbali zinachukuliwa katika kuhakikisha kuwa vyombo vya habari vinakuwa mawakala wa kulinda lugha ya Kiswahili, ambapo Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa kushirikiana na wadau wa Kiswahili limeendelea kuendesha semina, warsha, makongamano na kutoa elimu inayohusu matumizi fasaha ya Kiswahili kwa waandishi wa vyombo vya habari mbalimbali pamoja na kuandika makala na vijitabu maalum na kuvisambaza kwa wanahabari kuhusu matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni utambulisho na utamaduni wa Taifa letu na vile vile ndiyo lugha ya Taifa, waandishi wa habari wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha lugha hii inaendelezwa ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuzingatia matumizi sahihi.

Aidha, mifano iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge ya "wimbo huu" na "hiki" ni mada za nomino na sarufi ambazo hufundishwa katika somo la Kiswahili katika shule za msingi na upili. Hivyo, napenda kutoa wito kwa wanafunzi ambao miongoni mwao ni wanahabari watarajiwa kujifunza masomo yote kwa bidii ikiwa ni pamoja na Kiswahili.

Vilevile wamiliki wa vyombo vya habari wazingatie ufaulu wa somo la Kiswahili kama moja ya sifa kwa waombaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashauri wanahabari kutumia zana kama vile kamusi na vitabu vya miongozo ya uandishi na kuhudhuria makongamano ya Kitaifa na ya Kimataifa ya lugha ya Kiswahili, kwa mfano, Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA) na Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili Afrika Mashariki (CHAWAKAMA) ambayo hufanyika mwezi Septemba kila mwaka. Katika makongamano hayo, masuala ya kisarufi na ya kifasihi huwasilishwa na kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itawasaidia kuongeza ujuzi na weledi wa lugha ya Kiswahili, kujua pia istilahi za kisayansi na kiteknolojia na hivyo kuandika na kutangaza kazi bora na zenye maudhui lengwa kwa jamii na kuepuka upotoshaji wa maneno ya Kiswahili usio wa lazima. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa, swali la nyongeza.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Upo ushahidi wa matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa viongozi wa Serikali na miongoni mwetu Wabunge. Kwa sababu Bunge na viongozi wa Serikali ni miongoni mwa makundi ya jamii na taasisi zenye wajibu wa juu kabisa wa kulinda lugha hii na kwamba inaashiria tatizo hili haliko kwenye vyombo vya habari tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inasema nini kuhusu upana wa tatizo hili hasa kwa wakati huu ambapo inatengeneza sera hiyo?

Pili, kwa sababu matumizi, kwa mfano ya neno "hichi" badala ya "hiki," "nyimbo hii" badala ya "wimbo huu," uchanganyaji wa lugha ya Kiingereza kwa kiwango kilichokithiri kwenye sentensi za Kiswahili, vinakera. Tunaomba kujua ni lini sera hii inakuja kudhibiti hali hii inayoendelea? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mukasa, nadhani hilo tutaanza kudhibitiwa sisi wenyewe humu ndani, maana ndio tunaongoza kwa kuharibu lugha ya Kiswahili. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mbunge wa Biharamulo kwa jinsi ambavyo amejitahidi kuonesha ukinara katika kuikuza lugha ya Kiswahili. Naomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na matumizi ambayo siyo sahihi ya lugha yetu ya Kiswahili na wengi tumekuwa tukishuhudia kwa mfano "hiki kikao" wengine husema "hichi kikao," "hiki kitu", "hichi kitu" na pengine kama alivyosema katika maelezo yake kwenye swali lake la msingi, ni kwamba hata watoto kwa sasa ukifuatilia utaona, "hiki kitu" kwa sababu tunatumia "hichi kitu," sasa na wao wameanza kusema "hiko kitu." Wameibadilisha, badala ya "hiki kitu," sasa wanasema "hiko kitu."

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile siyo katika Kiswahili tu, watu wamekuwa wakichanganya Kiingereza, lakini hata lugha zetu za asili vilevile wamekuwa wakichanganya Kiingereza. Kwa mfano, unaweza kumsikia mtu anasema "*infact* kwa kweli *angambila nshomile*." Haya ni maneno ambayo yamekuwa yakichanganywa katika lugha za asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wito wa Serikali ni kwamba tulinde Kiswahili na pia tulinde lugha zetu za asili kwa sababu zile lugha za asili ndipo tunapoweza kupata maneno ya kuongeza kwenye Kiswahili pale ambapo tutakuwa hatuna maneno mbadala ya Kiingereza. Kwa hiyo, tulinde lugha zetu zote, lugha ya Kiswahili na pia lugha ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongezea tu ni kwamba Serikali ipo tayari kupitia BAKITA kuja kutoa semina katika Bunge hili ili kusudi tuweze wote kwa pamoja kufuatilia na kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Nalisema hili kutokana na kwamba kuna visababishi ambavyo vinapelekea matumizi yasiyo sahihi au visababishi ambavyo vinaweza kumwezesha mtu atumie lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika nchi za Afrika Mashariki wanaotumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya asili ni watu wapatao milioni mbili hadi milioni 15 kwa mujibu wa takwimu. Lakini wengi wao kuanzia milioni 50 hadi

milioni 150, wengi wanatumia Kiswahili kama lugha ya pili. Kwa hiyo, wakati mwingine inatokea tafsiri ya lugha zile za asili kwa Kiswahili.

Vilevile kuna kisababishi kingine ambacho ni jinsi gani ile lugha ya asili inashabihiana na lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, Kiswahili kina 'r' na kina "l" lakini zipo lugha ambazo hazina 'r' na hazina 'l'. Kwa mfano, kuna lugha moja ya asili isiyokuwa na 'r', akitaka kusema 'anataka kula' anasema 'nataka kura' na mwingine akisema naomba kura anasema 'naomba kula.' Kwa hiyo, hivi ni visababishi ambavyo vinapelekea matumizi sahihi au yasiyo sahihi kwa lugha ya Kiswahili.

Jambo lingine ni dhamira ya mtu ya kutaka kuwa kinara katika kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, tunavyomwona Mheshimiwa Rwegasira, yeye ana dhamira ya kutakakuwa kinara. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na viongozi tuwe na hii dhamira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ile tabia ya kujisomea vitabu vya Kiswahili, magazeti, kamusi pamoja na kutumia miongozo mbalimbali. Hivi vyote hupelekea mtu kuweza kuongea Kiswahili kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili linahusiana na Sera ya Lugha…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba ufupishe kidogo jibu linalofuata.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu inaendelea kukusanya maoni ya wadau kuhusiana na Sera ya Lugha ili kusudi kuweza kupata changamoto ambazo zinaikabili lugha yetu ya Kiswahili, lakini vile vile kujua ni jinsi gani tutazingatia masuala mbalimbali katika Sera ya Lugha na hivyo katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2016/2017 tunatarajia kwamba rasimu ya kwanza ya Sera ya Lugha itakuwa imekamilika na hivyo tuipeleke katika hatua za juu kwa ajili ya maamuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kuniona. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, kuna baadhi ya nyimbo zinazoimbwa katika ma-*stage show* au zinazooneshwa katika runinga. Nyimbo hizi huwa zinatudhalilisha wanawake kuvaa yale mavazi yao ambayo yanaonesha, je, Serikali inazingatia suala hili au kisheria ni sawa kuimba nyimbo kama zile zinazotudhalilisha sisi wanawake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kuhusiana na nyimbo ambazo zinadhalilisha wanawake ni swali jipya naomba alilete vizuri ili kusudi tuweze kulijibu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vyombo ambavyo vinasimamia kwa kupitia sheria zetu. Tuna Bodi ya Filamu ambayo huwa inaangalia, inapitia maudhui yenyewe kama ni ya filamu au wimbo, lakini pia tuna Kamati ya Maudhui ambayo ipo chini ya *TCRA*. Kwa hiyo, kwa kutumia sheria zetu tunadhibiti hali kama hii. Vilevile wale ambao wanaona kwamba hali hairidhishi, tunaomba wawasilishe ni wimbo upi au ni filamu ipi ili kusudi hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ufasaha wa lugha yoyote ile ni ajira na Kiswahili ni kimojawapo. Tanzania ni kitovu cha lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu Wizara ina mkakati gani wa kufunza na kutoa walimu wengi ambao wanaweza kupelekwa nchi mbalimbali, kwa mfano, Uganda, Rwanda sasa hivi wameanzisha Kiswahili kwenye shule zao na ninaamini Watanzania ndio wenye lugha fasaha ya Kiswahili. Je, kuna mkakati gani kufundisha walimu wa kutosha wa kuweza kuwapeleka nchi mbalimbali ambao wanazungumza Kiswahili na kutoa ajira kwa wananchi wetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri naona amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba kitovu cha Kiswahili ni hapa nchini kwetu Tanzania na kwa kulitambua hili, nchi za Afrika Mashariki wameamua Makao Makuu ya Kiswahili yawe hapa nchini na yamepelekwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa na tumekuwa tukizalisha Walimu wa Kiswahili wengi kadri inavyowezekana; na siyo tu kuwazalisha, lakini kuwatafutia soko na wamekuwa

wakipata masoko siyo tu katika Afrika na Afrika Mashariki, lakini hata nje ya nchi yetu na hasa China wamekuwa wakienda kwa wingi sana. Chuo Kikuu cha Zanzibar, kwa mfano *SUZA*, wamekuwa wakizalisha Walimu wengi sana wa Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia huu mchakato sasa wa utengenezaji wa Sera ya Lugha ambao utaipa nguvu kubwa Kiswahili kama lugha ya nchi yetu, tutaweka mikakati ya kutosha ndani mle na sheria baada ya sera kukamilika ambayo itatusaidia zaidi kukifanya Kiswahili kiendelee kuwa bidhaa na hivyo kuwapa soko kubwa walimu ambao tutakuwa tukiwazalisha nchini kwetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Wegesa Heche, Mbuinge wa Tarime Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Maeneo ya Wachimbaji Wadogo**

**MHE. JOHN W. HECHE** aliuliza:-

Kwa mujibu wa tafiti, uchimbaji mdogo ndio unaotoa ajira kwa wingi katika sekta ya madini:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika eneo la Nyamongo?

(b) Je, kwa kutokuwatengea vijana maeneo ya uchimbaji, Serikali haioni kuwa inazidisha chuki ya vijana dhidi ya mgodi wa *Acacia North Mara?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Wegesa Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 Serikali ilitenga eneo lenye ukubwa wa hekta 598 katika eneo la Nyamongo, Kitongoji cha Kerende kuwa eneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo; kadhalika katika eneo hilo ilitoa leseni 96 za uchimbaji mdogo kwa wananchi katika mwaka 2014, kadhalika Serikali ilitenga eneo la ukubwa wa hekta 49.18 katika Kijiji cha Nyakunguru

linaloweza kutoa leseni tano za uchimbaji ambapo hivi sasa leseni nne zimeshatolewa kwa Kampuni ya *Itandura Miners Cooperation Limited* ambayo ipo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo yametengewa eneo ni pamoja na eneo la Gorong'a ambayo ilitenga eneo la hekta 82.52 lenye leseni nane za uchimbaji mdogo ambapo leseni tatu kati ya hizo zimetolewa kwa wananchi wa eneo hilo. Katika eneo la Msege, Serikali pia ilitenga leseni tisa za uchimbaji mdogo kwa wananchi wa eneo hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wananchi wanapokosa maeneo ya uchimbaji wanaweza kuwa na chuki na wawekezaji wakubwa. Kwa kutambua hilo basi, Serikali imeendelea kuitekeleza azma hii ya kuwatengea maeneo wananchi ili wananchi wapate mahali pa kufanyia kazi na kuondoa chuki kati yao na wawekezaji wakubwa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya watu wa Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utofauti wa uelewa wa wachimbaji wadogo kati ya uelewa walionao Serikali na uelewa tulionao sisi wananchi na tunaokaa maeneo ya migodi. Tunapozungumzia wachimbaji wadogo, hatuzungumzii watu wajanja wajanja wanaoweza kwenda mjini wakapata leseni, wakarudi wakajiita wachimbaji wadogo. Tunazungumzia watu waliopo kule kijijini ambao ndio wanachimba kwa kutumia majembe, sururu na nyenzo nyingine ambazo ni duni.

Sasa swali langu, kuna maeneo ambayo yalikuwepo na watu wanachimba pale na bahati mbaya watu wanatoka kule vijijini wanakwenda Dar es Salaam wanapewa leseni, Serikali haishirikishi hata Serikali za Vijiji, wanarudi wanaondoa wachimbaji wadogo, kama eneo moja linaitwa Tigite, bwana mmoja ameondoa zaidi ya watu 20 pale. Sasa nataka Naibu Waziri anijibu, ni lini Serikali itatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo walioko kule vijijini, sio hawa wenye leseni wanaokwenda Dar es Salaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wakati Mgodi wa *North Mara* unaanza, ulitwaa eneo kwa maana ya ile leseni waliyopewa, walipewa eneo kubwa sana na kuna maeneo ambayo mpaka sasa hawayatumii na hawayafanyii kazi. Mojawapo ya eneo hilo ni *Serengeti Crossing.* Kwa nini Serikali isiuombe mgodi utoe lile eneo kwa wananchi kwa sababu mgodi

haulitumii kabisa, ili wananchi wafanye kazi pale wajipatie kipato na waendeshe maisha yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Heche jinsi ambavyo ameendelea kutupa ushirikiano katika masuala mbalimbali ya migogoro ya wananchi wa Nyamongo. Nakupongeza sana Mheshimiwa Heche. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, nijielekeze kwenye maswali yake ya nyongeza, ni lini Serikali itatenga maeneo katika maeneo mengine hasa katika eneo la Tigite ambalo amelitaja? Naomba tu mara baada ya kikao hiki nikutane na Mheshimiwa Heche atupatie maeneo kwa sababu Serikali bado inaendelea kuongea na mgodi ili ipate maeneo mengine kwa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, nitazungumza na Mheshimiwa Heche kuhusiana na hili ili eneo la Tigite alilotaja pia litengewe wananchi wa Nyamongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, kwanza tu nieleze kwamba Mheshimiwa Heche anavyosema kwamba *North Mara* imepewa maeneo makubwa, ni kweli, yapo maeneo ambayo Serikali inazungumza na mwekezaji ambayo ni makubwa na mgodi haujaanza kuyatumia. Tunafanya majadiliano, yakishakamilika, tutaongea na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kabla leseni hazijatoka, utaratibu tulioweka sasa ni pamoja na kushirikisha viongozi wa maeneo yale ili leseni itakapotoka waweze kutupa ushirikiano mkubwa. Kwa hiyo, eneo hili ambalo ni kubwa kwa wachimbaji wakubwa, tutazungumza na Mgodi wa *North Mara,* maeneo ambayo tutayapata Mheshimiwa Heche tutashirikiana na wewe ili wananchi waendelee kupelekewa maeneo zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, swali la nyongeza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza linalofanana na swali ambalo ameuliza Mheshimiwa John Heche.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kwangu kuna eneo lina dhahabu na kampuni moja inaitwa *Shanta Mining* imeingia na kupewa eneo hilo tangu mwaka 2004. Leo ni miaka 13 haijaanza kuchimba madini, haijajenga mgodi na

kwa taarifa za kitaalam ambazo nimeziangalia, hizo *deposits* za dhahabu siyo kubwa sana za kuweza kupewa kampuni ya kigeni. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri alieleze Bunge lako kama Serikali ina mpango wa kulitwaa hilo eneo na kuwarudishia wananchi ili wachimbaji wadogo wadogo wenyeji wachimbe kwa sababu baada ya miaka 13 hawachimbi, hawa wawekezaji inaelekea hawana mpango au uwezo wa kuchimba dhahabu kwenye hili eneo la Mang'oni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kwanza namshukuru Mheshimiwa Tundu. Nimekuwa nikiwasiliana naye mara kwa mara kuhusiana na kumpatia eneo. Niseme tu, ni kweli kabisa Kampuni ya *Shanta Mining* ilipewa leseni ya utafiti tangu mwaka 2004. Nieleze kidogo, muda wa kufanya utafiti kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya 2010, awali ya kwanza ni miaka minne, baada ya miaka minne anapewa tena miaka mitatu ya kuendelea na utafiti na hatimaye anamalizia miaka mitatu. Kwa hiyo, ni kweli kabisa shughuli za utafiti zinachukua muda mrefu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, baada ya kukamilisha utafiti, kampuni inatakiwa ianze shughuli za uchimbaji, hivi sasa kama ambavyo Mheshimiwa Tundu anasema haijaanza, matarajio ya mgodi ni kuanza shughuli za uchimbaji kati ya Juni, 2018. Kwa hiyo, baada ya shughuli za uchimbaji kuanza, basi maeneo mengine yata maeneo mengi yatashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yapo maeneo ambayo Kampuni ya *Shanta Mining* tunazungumza nayo. Hivi sasa tumezungumza na Kampuni ya *Shanta Mining,* inatarajia kuwa na maeneo ya hekta kama 200 ambayo inaweza ikawaachia wananchi wa Singida ili wachimbe kwa ajili ya uchimbaji mdogo kwa sababu yanaweza kuonekana siyo manufaa kwa kampuni hiyo. Baada ya taratibu hizo kukamilika, Mheshimiwa Tundu Lissu basi wananchi wako watawasiliana na Serikali tu na watapewa maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Geita walipewa magwangala *fake,* na kwa kuwa Sheria ya Leseni ya Uchimbaji Mkubwa inawataka wachimbaji wakubwa kila baada ya miaka mitano wamege baadhi ya eneo wawarudishie wachimbaji wadogo. Je, Wizara iko tayari sasa kulimega eneo la Nyamatagata na Samina kuwarudishia wananchi kuwafuta machozi kwa magwangala *fake* waliyopewa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Musukuma, katika jitihada ambazo ziliwasababisha wananchi wapewe magwangala ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, tunakupongeza Mheshimiwa Musukuma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitambue kwamba shughuli za utafiti na uchimbaji wa madini kwa kawaida kabisa, ni za kupata na kupotea. Sasa ni jambo la kawaida, mwekezaji anaweza akawekeza kwenye kuchimba na akakosa. Kama ambavyo ilikuwa kwenye magwangala, wananchi walitarajia pangekuwa na thamani, lakini bahati mbaya hapakuwa na thamani. Kwa hiyo, nilitaka tu kumwelewesha Mheshimiwa Musukuma na ninampongeza sana. Pia kwa wachimbaji wote, ni jambo la kawaida mchimbaji kuanza kuchimba na asipate madini ya thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu kusema, suala la Nyamatagata na Samina, ni kweli kabisa Serikali inazungumza na Mgodi wa *GGM* pamoja na wawekezaji wengine, hivi sasa tuko katika hatua nzuri. Mwaka 2016 Kampuni ya *GGM* ilirusha ndege kuangalia maeneo ambayo hayahitaji.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Musukuma nikuhakikishie kwamba mara baada ya taratibu hizi kukamilika, wananchi wa Nyamatagata na Samina, maeneo ambayo yataachiwa na mgodi, basi yatatengwa rasmi kwa ajili ya wananchi, lakini baada ya kukamilisha mazungumzo na mgodi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Bashe, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa maeneo mengi ambayo wawekezaji wakubwa wamewekeza wameacha athari kubwa katika maeneo hayo na mojawapo ni Wilaya ya Nzega katika Mgodi wa *Resolute,* wananchi wameachiwa mashimo

makubwa bila manufaa yoyote. Je, Serikali sasa iko tayari kumnyima mwekezaji Kampuni ya *Resolute, certificate* ya kumruhusu kuondoka nchini ambayo anatakiwa apewe mwezi wa sita kabla hajalipa deni ambalo anadaiwa la shilingi bilioni 10 na Halmashauri ya Mji wa Nzega? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Kampuni ya *Resolute* ilifunga mgodi wake miaka mitatu iliyopita. Katika utaratibu wa uchimbaji, mgodi unapoanza huwa kuna *Mine Closure Plan*. Kwa hiyo, wakati wanafunga mradi, kampuni ilitakiwa kutekeleza *Mine Closure Plan,* lakini sambamba na hilo, huwa inapewa *certificate* ya ku-*close* mgodi. Sasa Wizara ya Mazingira pamoja na *NEMC* wanalifanyia kazi suala hilo, watakapokamilisha taratibu Mheshimiwa Bashe utashirikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ni kwamba je, ni kwa nini Serikali haioni sababu ya kuwanyima *certificate?* Ni jambo ambalo namwomba Mheshimiwa Bashe avute subira, watu wetu wa *NEMC* na Mazingira wanalifanyia kazi. Nitambue ushiriki wako Mheshimiwa Bashe kwa wananchi wa Nzega. Niseme tu sambamba na hilo, ili kuwawezesha wananchi wa Nzega wapate maeneo na kuondokana na athari, mara baada ya taratibu za mazingira kukamilika, maeneo ambayo yaliachwa na *Resolute* ambayo yako wazi, yatamilikishwa kwa wananchi wako ili waweze kupata shughuli za kufanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 37

**Matumizi ya Maji ya Mto Malagarasi**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Katika Mto Malagarasi iko miradi mikubwa mitatu ambayo ni mradi wa kutoa maji Mto Malagarasi kwenda katika vijiji 69 vilivyopo Wilaya ya Urambo, uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji wa miwa na mradi wa uzalishaji wa umeme wa megawati 44.5.

(a) Je, Mto Malagarasi una ujazo gani wakati wa masika na kiangazi?

(b) Je, maji ya mto huo yanatosheleza mahitaji ya miradi hiyo mitatu?

(c) Je, Serikali imefanya utafiti wa kiufundi kujua bajeti ya maji katika mto huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia Mto Malagarasi, ikiwemo mradi wa maji kwa ajili ya Miji ya Urambo na Kaliua, kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji umeme wa megawati 44.5. Wakati wa masika mto huu unakuwa na maji yanayotiririka kwa mita za ujazo 55 kwa sekunde; na wakati wa kiangazi unakuwa na mita za ujazo 40 kwa sekunde.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Kwanza imekamilisha mipango ya pamoja ya uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji katika Bonde la Ziwa Tanganyika ambako Mto Malagarasi unapatikana. Hii ni sehemu ya utafiti wa kiufundi wa kujua wingi na ubora wa maji pamoja na mgawanyo sawia wa matumizi ya maji katika Bonde dogo la Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utafiti huo, umeonesha ya kuwa Mto Malagarasi una maji ya kutosha kwa miradi mbalimbali itakayoibuliwa ikiwemo miradi mitatu iliyotajwa na bado yatabaki kuelekea yakitiririka kwenda Ziwa Tanganyika.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya kiufundi yaliyotolewa na Naibu Waziri, nina maswali madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ikolojia ya Mto Malagarasi ina athari ya moja kwa moja kwa maji katika Mji wa Kasulu, nilitaka kufahamu ule mradi mkubwa unaofadhiliwa na Serikali ya India kwa takriban shilingi bilioni 9.89, ni lini mradi huo sasa utaanza kutekelezwa katika Mji wa Kasulu ili Kasulu yote na viunga vyake na miji midogo inayozunguka Mji wa Kasulu iweze kupata maji ya uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka kujua mkandarasi aliyekuwa anashughulikia mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kuyaleta katika Mji wa Kigoma amefilisika, na mmetangaza kwamba sasa anatafutwa mkandarasi mwingine, napenda pia kujua juhudi za kumpata mkandarasi mwingine badala ya huyu aliyefilisika kwa mradi wa Kigoma Mjini zimefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, suala la miradi kwa ufadhili wa Serikali ya India, hatua tuliyoifikia sasa tunafanya *shortlisting* kupata mhandisi mshauri atakayefanya usanifu wa kina kuweza kujua ni shughuli zipi zitafanyika katika Mji wa Kasulu, ndiyo fedha ziweze kutoka. Kwa hiyo, tupo kwenye hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu mkandarasi ambaye ana mradi mkubwa wa maji pale Kigoma Mjini, naomba nisiseme kwamba tunatafuta mkandarasi mwingine kwa sasa, kwa sababu bado hiyo kandarasi haijafutwa.

Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo tunafikiria *may be* tunaweza tukafanya, lakini tukisema sasa, inaweza ikaathiri utekelezaji wa mradi huu. Serikali itahakikisha kabisa kwamba mkataba uliyokuwepo utakamilisha ili wananchi wetu wa Kigoma waweze kupata maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kitwanga, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani huo ulikuwa ni uchaguzi mzuri mpaka Bunge zima linakubaliana na uchaguzi wa muuliza swali la nyongeza. Karibu. *(Kicheko)*

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba niulize swali la nyongeza.

Natambua kwamba chanzo cha maji Ihelele ndicho kinachopeleka maji katika Mji wa Shinyanga na Kahama; lakini tangu tumepewa ahadi ya kuwekewa maji katika vijiji hivyo mwaka 2008 maji hayatoki mpaka leo. Sasa Serikali ina mpango gani, maana wananchi wanasema kama hakuna mpango

mkakati, tutaungana na mimi nitaungana nao kwenda kuzima mtambo wa maji wa kwenda Shinyanga. Nitawasindikiza wananchi kwenda kuzima. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kasi mpya hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais mwaka 2008 alitoa ahadi ambayo itahakikisha eneo lote la Ihelele linapata maji ya kutoka KASHWASA. Baada ya ahadi hiyo; na kwa kwa mujibu wa taratibu za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, tulianza kufanya utafiti na utafiti huo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba umekamilika. Ili kuweza kusambaza maji katika eneo lako la Ihelele tunahitaji shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hii bajeti sasa ambayo tunaiandaa sasa hivi ya mwaka 2017/2018, basi tutaanza kutenga fedha ili kutekeleza sasa mradi wa kuwapatia wananchi maji Ihelele kutoka kwenye huo mradi wa KASHWASA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa ahadi hii yeye na wananchi wake hamna haja ya kufunga yale maji kwa sababu tunawaletea maji. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Ufunguzi wa Nyayo za Laetoli**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA,** aliuliza:-

Tarehe 25 Oktoba, 2016 Kituo cha Televisheni cha Mlimani TV kilirusha Kipindi cha Urithi Wetu kilichozungumzia Malikale za Taifa letu na namna ambavyo agizo la Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete la ufunguzi wa nyayo za Laetoli linavyosuasua kutekelezwa kwa kisingizo cha ukosefu wa wataalam.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuajiri wataalam hao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nyayo za Laetoli zilizogunduliwa na mtafiti Dkt. Mary Leakey mwaka 1978 katika eneo la Laetoli katika Hifadhi ya Ngorongoro ni ushahidi wa pekee duniani usiopingika kwamba binadamu wa umri wa miaka milioni 3.6 iliyopita waliweza kutembea wima kwa miguu miwili katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2007 aliagiza Wizara yangu kufukua nyayo hizo na kuzihifadhi kwa njia ya kisasa itakayoruhusu matumizi ya elimu na utalii kwa Watanzania na wageni na kwamba Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro igharamie kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unakadiriwa kugharimu takribani Dola za Marekani milioni 50 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 105. Fedha hizo zitatumika kuwasomesha wataalam, kuandaa michoro ya ujenzi wa makumbusho, kufukua na kuhifadhi nyayo, kusimamia ujenzi na kuweka mifumo ya uhifadhi. Fedha hizo ni nyingi ukilinganisha na mapato na majukumu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Hivyo Wizara yangu inaendelea na jitihada za kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kugharamia utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba hakuna hali ya kusuasua katika katika utekelezaji wa mradi huu muhimu na kwamba baadhi ya kazi zimekwishakamilika na nyingine ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizokamilika ni pamoja na kuundwa kwa Idara ya Urithi wa Utamaduni, kukamilika kwa michoro ya awali ya jengo la mapokezi, jengo la utafiti na jengo la elimu kwa umma, kuwasilishwa kwa tathmini ya athari kwa mazingira kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na *UNESCO* kwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kutoa idhini na mafunzo ya shahada ya uzamivu kwa watumishi wawili.

Kazi ambazo zinaendelea kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha taratibu za ajira kwa baadhi ya wataalam wanaopatikana nchini na ukusanyaji wa takwimu sahihi kuhusu mazingira rafiki ya nyayo hizo kazi ambayo inafanywa na wataalam kutoka nje ya nchi na inatarajiwa kukamilika mwezi Februari 2017 na

kwa maana hiyo, napenda kusema kwamba kazi hii imekwishakamilika kwa sababu tulikuwa tumepanga ikamilike mwezi huu, mwaka 2017.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu naona umekaa, kwa hiyo, umeridhika. Mheshimiwa Semesi. Mheshimiwa Hawa Mchafu una swali la nyongeza?

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Nina swali la nyongeza eeh.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa nasubiri umalize kwanza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba sasa nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Maendeleo ya Dunia ya mwaka 2010 inaitaja Tanzania kama nchi yenye malikale adimu na urithi wa utamaduni wa Taifa ambao ungeweza kuongezea nchi yetu kipato na kukuza uchumi wetu. Nataka kujua sasa, Tanzania inafanya nini katika kutumia malikale zake hizo adimu kama Olduvai Gorge, Laetoli, Kolo na Kilwa Kisiwani ili iweze kuiongezea nchi yetu kipato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuzingatia umuhimu na mchango wa malikale za Taifa letu katika kukuza uchumi, mnamo mwaka 2007 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliagiza nyayo hizo ziweze kufukuliwa ili watalii wengi zaidi waweze kutembelea eneo hilo na nchi yetu iweze kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, anasema hakuna kusuasua kwa ufukuzi wa nyayo hizo ilhali sasa hivi inapita miaka 10 tangu agizo hilo litolewe na hadi hivi sasa tunavyozungumza, bado nyayo hizo hazijafukuliwa. Kwa hiyo, ninachotaka kujua, wananchi wa maeneo yale ambao wanazungukwa na ile *historical site* wananufaikaje kwa uwepo wa hiyo *historical site?* Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Chakoma kwamba Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba maeneo yetu haya ya urithi wa Taifa yanaletwa katika kiwango ambacho kinaweza kutumika na kutuzalishia mapato katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Ngorongoro, eneo hilo limefukuliwa na wataalam kutoka Tanzania, Spain pamoja na Marekani na kuvumbua nyayo nyingine ambazo zinaonesha kwamba wanadamu hao wanaitwa Zamadamu, walikuwa wanaishi pale wakiwa wanatembea *upright* miaka milioni 3.6 iliyopita. Nyayo hizo mpya ambazo ziligundulika, zilifunguliwa mwezi Machi, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo pia linajenga *museum* kubwa, eneo la mapokezi, maktaba na kuonesha vitu mbalimbali ambavyo vitavutia sana watalii watakaotembelea eneo hilo. Aidha, Serikali inaendelea kuyafufua na kuyakarabati maeneo mengi ya Malikale ambayo Mheshimiwa Chakoma ameyataja na kwamba maeneo haya yakiwekwa katika utangazaji wetu wa utalii yatakuwa na mvuto mkubwa na yataongeza mapato ya Serikali kwa kiwango kikubwa sana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Susan Lyimo, tafadhali.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Ukosefu wa Ofisi na Vitendea Kazi kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji - Njombe**

**MHE. LUCIA M. MLOWE** aliuliza:-

Jeshi la Zimamoto Mkoani Njombe linakabiliwa na ukosefu wa Ofisi pamoja na vitendea kazi hususan magari jambo linalopelekea Jeshi hilo kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Je, ni lini Serikali italipatia Jeshi hilo ofisi za kudumu pamoja na magari ili liweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina uhaba mkubwa wa ofisi na vitendea kazi katika vituo vyote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuongeza bajeti kwa Jeshi la Zimamoto na uokoaji ili liweze kukabiliana na changamoto zilizopo zikiwemo uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya kuzimia moto, magari ya maokozi pamoja na kufanyia ukarabati ofisi zilizopo katika mikoa yote na kuliwezesha Jeshi la Zimamoto kuwa la kisasa ili kutoa huduma nzuri kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nia hii njema ya Serikali itakuwa ikitekelezwa kwa mujibu wa upatikanaji mapato ya Serikali na bajeti itakayotengwa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kila mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucia Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sijaridhika kabisa na majibu ya Naibu Waziri, Jeshi la Zimamoto linafanya kazi katika mazingira magumu sana. Mfano, Mkoa wangu wa Njombe hawana ofisi, wanatumia majengo ya Idara ya Maji, hawana magari; na tukiangalia Mkoa wa Njombe kijiografia umekaa vibaya sana na matukio ya moto ni mengi.

Nilikuwa nataka kujua *time frame,* ni lini Serikali itatoa vifaa au vitendea kazi kwa Jeshi la Zimamoto?

Swali langu la pili, kwa kuwa huduma ya Zimamoto iko zaidi mijini, lakini matatizo ya moto yako mengi sana vijijini. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha hata watu wa vijijini wanapata huduma hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi kwamba tuna matatizo ya ofisi pamoja na vitendea kazi nchi nzima kwa Jeshi la Zimamoto; na ukiangalia katika Wilaya zote takribani za nchi nzima kwa upande wa Tanzania Bara ni Wilaya 20 ambapo kuna Ofisi za Zimamoto mpaka sasa hivi pamoja na magari.

Hata hivyo, Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba tunatanua wigo ili huduma hizo ziweze kufika mpaka vijijini na ndiyo maana tuna mpango sasa hivi wa kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma za Zimamoto katika Wilaya zote nchini hatua kwa hatua kwa kuanza kupeleka Maofisa ili waweze kutoa elimu na baadaye kadri vifaa vitakavyopatikana tutapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na magari pamoja na vitendea kazi, katika bajeti ya mwaka huu tumetenga takriban shilingi bilioni 1.5 kununua magari mawili, tutaangalia ni maeneo gani ya kipaumbele tuweze kupeleka.

Naomba nichukue fursa hii kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashauriana na Makao Makuu Idara ya Zimamoto tuone uharaka wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna mpango mwingine, tunafanya mazungumzo sasa hivi na Austria pamoja na Belgium, Kampuni ya *SOMAT* ya Belgium ili kuweza kupata mkopo wa *Euro* bilioni tano pamoja na *Euro* milioni 1.9 ambazo zitasaidia kuweza kununua vifaa viweze kupunguza makali ya upungufu wa vifaa katika maeneo mbalimbali nchini mwetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Freeman Mbowe swali la nyongeza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani inakabiliwa na upungufu mkubwa wa magari na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukiri kwamba wanapungukiwa sana magari, vitendea kazi pamoja na ofisi. Vilevile wana upungufu mkubwa wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu, siku za karibuni, kwenye upande wa Jeshi la Polisi ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani pamejitiokeza utaratibu ambapo Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanalitumia Jeshi la

Polisi kuwalinda wao binafsi wakati kuna matatizo makubwa ya kiulinzi katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu ni hili, nikitoa mifano halisi, katika Mkoa wa Arusha, Mkuu wa Mkoa wa Arusha analindwa na *section* nzima ya Jeshi la Polisi, ana *motorcade*, ana ving'ora asubuhi mpaka usiku. Sasa magari kama mawili au matatu yanamhudumia Mkuu wa Mkoa na *section* nzima ya Jeshi la Polisi ambayo ina askari tisa na ving'ora na hata Wakuu wa Wilaya wamejipa utamaduni huo sasa.

Je, ni nini itifaki ya Kitaifa kuhusu ulinzi wa Viongozi kama hata hawa Mawaziri wenyewe hawalindwi na Askari, lakini Wakuu wa Mikoa leo wanajilundikia Askari badala ya Askari kwenda kwenye lindo, ma-*OCD* wote siku hizi hawafanyi kazi ya ulinzi wanafanya kazi ya kulindana na kufuatana na Wakuu wa Wilaya. Tunaomba Wizara watueleze leo, ni nini sera ya Serikali kuhusu itifaki hii na matumizi mabaya ya Jeshi la Polisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwenye utendaji wa kazi kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya, Mkuu wa Mkoa ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, panapokuwepo na jukumu hasa ambalo linapohusisha shughuli za kiulinzi na nje ya ofisi, ni sahihi Mkuu wa Mkoa ama Mkuu wa Wilaya kuambatana na timu yake kwenda katika eneo husika. Inapotokea Mkuu wa Mkoa anakwenda ofisini kwake ama Mkuu wa Wilaya anakwenda ofisini kwake, maana yake *OCD* ama *RPC* ama wengine na wenyewe watakuwa kwenye ofisi zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi kwa mazingira ambayo nimekuwa nikipewa ni pale ambapo hawa viongozi wanakwenda katika eneo la tukio ambalo linahusisha ulinzi na usalama. Huo ndiyo muogozo kwamba kama wanaelekea katika eneo ambalo linahusisha ulinzi na usalama ni sahihi viongozi hawa kwenda na timu zao kwa sababu ni mambo ya kiusalama na sehemu ya kutolea maelekezo, lakini siyo wakati wa kwenda ofisini *on daily routine, unless* kama wanafanya hivyo itakuwa maeneo ambayo kila mmoja anaenda kwenye ofisi na ofisi hizo ziko katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, kwa maelekezo haya, ni kwamba viongozi hawa wanapokwenda kwenye majukumu ambayo yanahitaji maelekezo na ni ya kiulinzi na usalama na wao ndio Wenyeviti wa Ulinzi na Usalama itifaki inataka hawa watu wawe na hao viongozi kwa ajili ya maelekezo ya *site,* lakini wanapoenda kazini na hawa viongozi wengine nao wanaendelea na majukumu yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Oliver Daniel Semguruka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Usalama wa Raia wa Mpakani Mwa Rwanda, Burundi na Uganda**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Mkoa wa Kagera umezungukwa na nchi za Rwanda, Burundi na Uganda na mipaka ya nchi hizo imekuwa adhabu kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera, kwani hali ya usalama wa raia na mali zao umekuwa mashakani kutokana na kuvamiwa na majambazi toka nje ya Tanzania wakishirikiana na baadhi ya Watanzania wasio na uzalendo na Taifa lao.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuimarisha ulinzi katika mipaka hiyo ili wananchi wa Mkoa wa Kagera waweze kuishi kwa amani na utulivu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yako matukio ya ujambazi katika mikoa ya pembezoni ikiwemo Kagera ambapo watu toka nchi jirani wanaingia na silaha kali za kivita na kufanya unyang'anyi wa mali za wananchi. Hii inatoka na mkoa huu kupakana na nchi ambazo zimekosa amani na kuzalisha wahamiaji haramu kuingia nchini kwetu kwa njia za panya na tukizingatia kwamba mipaka yetu imezungukwa na mapori makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama inafanya mikakati ya kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya operesheni za pamoja katika mipaka yetu; vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi yetu na nchi ya jirani vinafanya operasheni za pamoja na kubadilishana taarifa mbalimbali za uhalifu na wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya ulinzi na usalama hufanya misako ya kushitukiza katika mapori yote yaliyoko Kagera, Kigoma na maeneo yote ya mipakani, kwani ndiyo maficho ya uhalifu; hufanya doria na polisi kusindikiza magari katika baadhi ya maeneo tete; Kamati za Ulinzi na Usalama za maeneo husika zinafanya vikao vya ujirani mwema ili kuwaelimisha wananchi juu ya kutoa taarifa kwenye Mamlaka za Serikali husika wanapoona wageni wasiofahamika wanaingia ama kutoka katika maeneo yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi la Polisi lina uhaba wa vitendea kazi vya kisasa kuweza kudhibiti matukio ya uhalifu; je, Serikali ina mpango gani kutoa vifaa vya kisasa zaidi kwa askari wetu waliopo katika maeneo ya mipakani?

Swali langu la pili; ili askari aweze kufanya kazi zake na kudhibiti matukio ya uhalifu kwa ufanisi ni muhimu akawa na mazingira rafiki kuanzia nyumbani.

Je, ni lini Serikali itatekeleza kwa vitendo ahadi ya kujenga makazi ya hadhi ya askari wa Jeshi la Polisi katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa na *concern* ya hali ya usalama katika mpaka wa Kagera, lakini naomba tu nimthibitishie kwamba, si Jeshi la Polisi ama Serikali kupitia Jeshi la Polisi kwa kutambua umuhimu na unyeti wa maeneo ya nchi yetu yaliyoko mipakani ikiwemo Kagera huwa kwa kawaida inatoa kipaumbele katika ugawaji wa vifaa katika maeneo hayo hususan vitendea kazi ikiwemo silaha, magari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni kwamba, kwa Mkoa wa Kagera pekee tunahakikisha kwamba tunawapatia Askari wetu walioko mipakani silaha za kutosha lakini silaha nzito ili kuweza kukabiliana na wimbi la wahamiaji haramu ambao mara nyingi wamekuwa wakisababisha ukosefu wa amani katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hakuna hata Kituo kimoja cha Polisi katika mipaka ya nchi yetu ambacho hakina gari mpaka sasa hivi tunavyozungumza. Kwa hiyo, ni kuonesha kwamba tunatoa nguvu kubwa sana na kipaumbele katika maeneo ambayo yapo mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili ni kweli kuna matatizo ya makazi, sio tu Kagera lakini katika mikoa mbalimbali nchi nzima na ndiyo maana tumekuwa tukizungumza hapa kuna mipango ya Serikali ya ujenzi nyumba 4,136 ambayo mpaka sasa hivi tunasubiri *approval* kutoka Hazina ili mradi ule uanze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kagera, kuna ujenzi wa nyumba 12 ambazo tunaendelea nazo hatua kwa hatua kadri ya pesa zitakazopatikana tumalize katika eneo la Buyekera ambalo litasaidia kupunguza makali ya matatizo ya makazi kwa askari wetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alex Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ni majibu ya Serikali. Lakini kwa kuzingatia kwamba Ngara ni miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Kagera, Wilaya inayopakana na nchi mbili, Rwanda na Burundi imekuwa ni waathirika wakubwa sana wa hali ya usalama katika eneo hilo. Sasa swali langu, je, ni lini sasa Serikali itaanzisha Kanda Maalum ya kipolisi kwa Wilaya hii ya Ngara ambayo kwa muda mrefu wamekuwa ni waathirika wa hali ya usalama? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumekuwa tukiangalia maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kubwa sana za kiusalama nchini mwetu na maamuzi ya kuongeza Wilaya katika maeneo hayo yanatokana na wingi wa matukio ya uhalifu. Ngara ni moja kati

ya sehemu ambayo kuna matukio ya uhalifu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, hasa kutokana na kupakana na nchi jirani. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge atuachie hili tunalifanyia kazi na baadaye pale ambapo hatua itakapofikiwa, tutamjulisha.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Serikali Kuhamisha Kivuko cha MV Kilombero II**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Mitambo wameahidi kuhamishia kivuko cha *MV* Kilombero II kwenda katika kivuko cha Kikove katika Mto Kilombero Juu (Mnyera) baada ya kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Kilombero.

Je, ni lini matayarisho ya uhamisho wa Kivuko hicho yataanza rasmi kwa kuwa ujenzi huo wa daraja la Kilombero unatarajia kukamilika hivi karibuni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)*, imeanza maandalizi ya kuhamisha vivuko vya *MV* Kilombero I na *MV* Kilombero II kuvipeleka eneo la Kikove katika Mto Kilombero kwenye barabara inayounganisha Mlimba na Malinyi. Wakala wa Barabara kwa kushirikiana na Wakala wa Ufundi na Umeme umefanya ukaguzi wa barabara ya Mlimba hadi Malinyi ili kubaini mahitaji ya miundombinu itakayowezesha kivuko hicho kufanya kazi katika eneo hilo la Kikove. Miundombinu hiyo ni pamoja na maegesho na barabara unganishi katika kila upande wa mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuhamisha vivuko vilivyopo eneo la Ifakara kwenda eneo la Kikove katika barabara ya Mlimba – Malinyi mara tu baada ya mradi wa ujenzi wa daraja la Mto Kilombero na barabara za maingilio kukamilika. Hivi sasa ujenzi wa daraja la Mto Kilombero

umekamilika na Mkandarasi anakamilisha ujenzi wa barabara za maingilio ili daraja lianze kutumika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya wakazi wa Wilaya ya Malinyi, Wilaya ya Ulanga na Kilombero, tunaishukuru Serikali na tunawapa pongezi kutekeleza ahadi ambayo wametuahidi ya ujenzi wa daraja la Kilombero ambayo imekuwa jawabu kubwa la kero ya miundombinu katika Wilaya hizo tatu. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ujenzi huo wa daraja la Kilombero unahusisha pia na barabara za maingilio na barabara hiyo ya maingilio inaunganisha barabara inayotoka Ifakara, Lupilo, Malinyi, Kilosa Mpepo, Londo, Lumecha, Namtumbo mpaka Songea. Barabara hii kipindi cha masika inachafuka sana kutegemea na mazingira ya mvua maeneo yale na inakuwa inapitika kwa tabu sana. Sasa, je, Serikali inajipangaje na ukarabati wa kudumu wa maeneo korofi katika barabara hiyo niliyotaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; barabara hii niliyotaja inajulikana kwa T16, barabara hiyo iko katika upembuzi yakinifu unaosanifu kwa kina ambao umekamilika. Barabara inatakiwa ijengwe kwa kiwango cha lami. Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hiyo inayotoka Ifakara, inatobokea mpaka Songea ambayo itakuwa sio kwa ajili ya mkaazi wa Morogoro itasaidia pia na ndugu zetu majirani wa Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Njombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea kwa niaba ya Serikali pongezi alizotupa na kwa kweli ni wajibu wetu kutekeleza ahadi zote ambazo tumezitoa katika Ilani ya Uchaguzi ya 2015/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayoongelea nayo iko katika Ilani ya Uchaguzi ya 2015 hadi 2020 ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Upembuzi na usanifu wa kina haujakamilika – *physically* umekamilika lakini taarifa bado

haijakamilika na tunatarajia hiyo kazi itakamilika mwezi Mei, 2017. Kwa sasa taarifa ya rasimu imeshawasilishwa *TANROADS* wanaipitia kwa kina ili hatimaye wamrudishie maoni yule Mhandisi Mshauri ambaye ni kampuni ya *Kyong Dong* na baada ya hapo ndio atakuja kukamilisha kuandika taarifa ya mwisho. Kwa ratiba ilivyo ataiwasilisha taarifa ya mwisho mwezi Mei, 2017. Baada ya hapo Serikali itaanza kujipanga kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la ukarabati wa maeneo korofi kwa sasa ili iweze kupitika muda wote; nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda Mbunge wa Malinyi na wananchi wote wa Malinyi hadi Kilosa kwa Mpepo kwamba Serikali ina mkakati kabambe na kila mwaka tunatenga fedha na nafahamu mwaka huu kuna wakandarasi wawili wako *site* katika maeneo korofi wanafanyia ukarabati wa hali ya juu ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika mwaka mzima bila matatizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kukamilika kwa daraja la Mto Kilombero ni wazi kwamba sasa Mkoa wa Morogoro unafunguliwa kibiashara. Nini mipango ya Serikali kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Lindi kwa barabara inayopitia kutoka Liwale kuelekea Morogoro? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kiongozi wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa ni moja kati ya ahadi yake ya kuhakikisha barabara kutoka Ilonga hadi Liwale inashughulikiwa. Ahadi hiyo tumepewa na nimhakikishie kwamba tutaishughulikia hadi tuikamilishe katika kipindi hiki cha miaka mitano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leonidas Gama, swali la nyongeza.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali juu ya ujenzi wa daraja la Kilombero lakini ahadi ya Serikali ya kukamilisha ujenzi wa barabara kupitia daraja la Kilombero kwenda Songea kupitia Namtumbo ni ya muda mrefu sana na hivi sasa wananchi wa Songea ukitaka kusafiri kwa kawaida ni masaa 15 kutoka Dar es Salaam mpaka

Songea. Hii barabara kutoka Kilombero kukatiza Namtumbo kwenda Songea ingerahisisha sana na usafiri ungekuwa mwepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri Serikali itupe majibu ni lini tunatazamia tuanze ujenzi wa barabara hii ya kuelekea Songea kupitia Kilombero? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hoja ya kujenga barabara hii ilianza toka mwaka 1996, tunafahamu. Tatizo lililokuwepo katika kipindi kirefu sana tulikosa fedha lakini hatimaye katika kipindi hiki na Serikali hii ya Awamu ya Tano naomba nimhakikishie kwamba kazi hii itafanyika muda si mrefu na kwa vyovyote ni ndani ya kipindi cha miaka mitano ambayo ahadi imetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu, akiangalia kitabu chetu cha Ilani atakuta hii barabara imeandikwa itajengwa kwa kiwango cha lami na hatua za mwanzo ndio hivyo tunazikamilisha mwezi Mei na baada ya hapo tunaanza utaratibu wa kutafuta fedha za kujenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine vile vile mimi mwenyewe natoka Namtumbo na nimetoa ahadi kwamba barabara hii mwaka huu lazima itoboke, isipotoboka *TANROADS* watatoboka! Kwa hiyo, nimhakikishie suala la kutoboa barabara hii, itatoboka mwaka huu, lakini kuanza ujenzi ni baada ya miaka ijayo ya fedha. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani mnajua utaratibu. Naomba mkae tafadhali. Spika ama kiti kikiwa kimesimama wote mnapaswa kukaa.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo halafu nitatoa maelezo kidogo kuhusu ratiba yetu ya leo.

Tangazo la kwanza linahusu wageni. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, tunayo makundi mawili. Kundi la kwanza ni wageni waliopo jukwaa la Spika na hawa ni Wajumbe saba na Katibu mmoja wa Kamati ya Kinga na Maadili ya

Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Ussi Yahya Haji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge lakini pia na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kututembelea kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Wageni wetu karibuni sana Bungeni.

Ninalo pia tangazo moja la kazi. Tangazo linatoka kwa Meneja wa Bunge *Sports Club* Mheshimiwa John Kadutu, anawatangazia Bunge *Spots Club* kuwa mazoezi ya *football* yanafanyika katika uwanja wa Chuo Kikuu cha *St. Johns* na *netball* mazoezi yanaendelea katika uwanja wa Jamhuri. Mazoezi yote yanaanza saa 12 asubuhi. *Manager* wa Bunge *Sports Club* anawakumbusha kuhudhuria mazoezi hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nimesema nitatoa maelezo kidogo. Leo kwa ratiba tuliyokuwa tumepewa siku ya Jumatatu ilikuwa tuwe na mjadala kuhusu Muswada wa Sheria wa Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi (2016). Mheshimiwa Spika, amepokea maombi ya Serikali kuhusu kuuondoa Muswada huo kwa sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

**WABUNGE FULANI:** Aaah! Kuna miongozo ya Waheshimiwa Wabunge.

**WABUNGE FULANI:** Kaeni chini.

*(Saa 5.20 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*